Ninapenda kunywa chai. _____

ZOEZI LA NNE - EXERCISE FOUR

TAFSIRI SENTENSI HIZI. TRANSLATE THE FOLLOWING SENTENCES INTO SWAHILI.

EXAMPLE: We all like beer.
Sisi sote tunapenda pombe.

1. We all want pork.
2. Anyone can drink the milk.
3. Do all the children like eating bread.
4. All of you want eggs?
5. He is reading the whole book.
6. She is cooking the whole cabbage.
7. I don't want anything to drink.
8. I don't like anybody.
9. Mother can eat anything.

ZOEZI LA PILI - EXERCISE FIVE

ANDIKA SENTENSI HIZI UKITUMIA WAKATI UJAO.
WRITE THE FOLLOWING ESNTENCES USING THE FUTURE TENSE.

For Example: Ninapika ugali na sukuma wiki.
Nitapika ugali na sukuma wiki.

1. Leo mama anapika wali na kuku.
2. Tunahitaji maji na unga kupika ugali.
3. Unaongeza kiasi kidogo cha maji.
4. Mpishi anapika chakula gani?
5. Kabla ya kuweka sukuma unaweka mafuta.
6. Unatumia mafuta gani?

ZOEZI LA SITA - EXERCISE SIX

TAFSIRI SENTENSI HIZI KWA KISWAHILI. TRANSLATE THE FOLLOWING SENTENCES INTO SWAHILI.

1. Yesterday I drank milk.
2. We ate Githeri in the evening.
3. She drank fruit juice.
4. You drank cold beer.
5. He refused to eat bread without butter.
6. The child did not finish his food.
7. The students didn't like breakfast.
8. The visitors were very satisfied.
9. We were very drank after the party.

MAELEZO YA UTAMADUNI - CULTURAL EXPLANATION:

In Kenyan culture it is considered rude to smell food. It is also considered very rude to put your hands in food especially while cooking. Not even when tasting do we put our fingers in food or lick the spoons we are using and then deep it back into the pot.

BEST COPY AVAILABLE

SOMO LA NANE

KUAGIZA CHAKULA - ORDERING FOOD

MAZUNGUMZO YA KWANZA - FIRST DIALOGUE

Weita: Hujambo bibi?
Njeri: Sijambo bwana.
Weita: Unataka kula nini.
Njeri: Kuna chakula gani?
Weita: Kuna ugali, nyama ya ng'ombe, nyama ya mbuzi, wali, chapati, kienyeji, kuku, samaki na mboga.
Njeri: Niletee nyama ya mbuzi na kienyeji.
Weita: Utakunywa nini?
Njeri: Kuna soda baridi?
Weita: Ndiyo.
Njeri: Niletee soda ya fanta baridi.
Weita: Chukua soda lakini, chakula utangojea kidogo.
Njeri: Sawa tu asante.

MAZUNGUMZO YA PILI - SECOND DIALOGUE

Daudi: Habari yako bwana?
Weita: Njema.
Weita: Umeagiza au bado?
Daudi: Sijaagiza, niletee menu.
Weita: Unataka kula nini?
Daudi: Niletee nyama ya mbuzi na viazi.
Weita: Utakunywa nini?
Daudi: Kuna pombe baridi?
Weita: Ndiyo, unataka gani?
Daudi: Nipe Tusker baridi.
Weita: Ngapi?
Daudi: Ni bei gani?
Weita: Shilingi kumi na tano.
Daudi: Chukua.
Weita: Asante. kwaheri.

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD

Nimeagiza.	Sijaagiza.
Umeagiza.	Hujaagiza.
Ameagiza.	Hajaagiza.
Umeagiza nini?	Nimeagiza chapati.
Tumeagiza.	Hatujaagiza.
Mmeagiza.	Hamjaagiza.
Wameagiza.	Hawajaagiza.

Niletee chai.
Mletee soda baridi.
Tuletee kahawa.
Waletee maziwa moto.

BEST COPY AVAILABLE

MENU
HUJAMBO? UNGEPENDA KULA NINI LEO?
NILETEE WALI, KUKU NA MBOGA TAFADHALI. PIA NIPE SODA BARIDI.
1
2
3

WEITA! NJOO HAPA TAFADHALI.
CHAKULA NI PESA NGAPI? NIPE RISITI TAFADHALI.
CHUKUA BILI YAKO.
1
2
3

Niletee kisu na uma.
Mletee glasi ya maji.
Tuletee sahani moja ya kienyenji.
Tafadhali, waletee maji baridi.

Nipe chai na mkate.
Mpe kikombe cha chai.

Tupe nyuma na vijiko.
Wape sukari na maziwa.
Nipe chakula, ninasikia njaa.
Tupe maji baridi, tunasikia joto sana.

Nimeagiza nyama, tafadhali niletee haraka.
Tumeagiza pombe baridi, tafadhali tuletee.
Hatujaagiza chakula, tumeagiza soda na pombe baridi.
Mmeagiza nini?
Tumeagiza ugali na mboga.

MSAMIATI SWAHILI		MSAMIATI PLURAL	VOCABULARY ENGLISH EQUIVALENT
agiza	(v)	-	order
sahani	(n)	sahani	plate
kisu	(n)	visu	knife
uma	(n)	nyuma	fork
glasi	(n)	glasi	glass
Kikombe	(n)	vikombe	cup
leta	(v)	-	bring
kupa	(v)	-	give
sikia	(v)	-	feel
moto	(adj)	-	warm
baridi	(adj)	-	cold
pombe	(n)	pombe	beer
zoezi	(n)	mazoezi	practice
maliza	(v)	-	finish
hoteli	(n)	hotel	hotel
mkahawa	(n)	mikahawa	restaurant
haraka	(adv)	-	quickly
pumzika	(v)	-	rest
soma	(v)	-	read
shiba	(v)	-	be full
fahamu	(v)	-	understand

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION:

THE PERFECT TENSE "ME"

The Perfect tense is used to show a completed action. It can be compared with the English tense "Have" and "Has". Therefore the English construction such as "I have eaten, you have eaten, he or she has eaten, is expressed as follows in Swahili.

Positive Singular

Nimekula - I have eaten.
Umekula - You (sing) have eaten.
Amekula - S(he) has eaten.

Negative Singular.

Sijakula - I have not eaten.
Hujakula - You (sing) have not eaten.
Hajakula - He/She has not eaten.

Positive Plural

Tumekula - We have eaten.
Mmekula - You (pl) have eaten.
Wamekula - They have eaten.

Negative Plural

Hatujakula - We have not eaten.
Hamjakula - You (pl) have not eaten.
Hawajakula - They have not eaten.

Note:

The negative of "ME" tense is "JA". When used with monosyllabic verbs, they drop their infinitive "KU" in the negative.

N.B. For further information on adjectives, refer to P.M. Wilson Page 40 - 44.

A: MONOSYLLABIC VERBS

AFFIRMATIVE SINGULAR		NEGATIVE
Nimekula.	-	Sijala.
Umekula.	-	Hujala.
Amekula.	-	Hajala.
Hatujashiba.	-	We are not full.
Hamjashiba.	-	You (pl) we are not full.
Hawajashiba.	-	They are not full.

PLURALS

Tumekunywa.	-	Hatujanywa.
Mmekunywa.	-	Hamjanywa.
Wamekunywa.	-	Hawajanywa.

POLYSYLLABIC VERBS

AFFIRMATIVE SINGULAR	NEGATIVE
Nimeshiba.	Sijashiba.
Umeshiba.	Hujashiba.
Ameshiba.	Hajashiba.

PLURALS:

Tumemaliza.	Hatujamaliza.
Mmemaliza.	Hamjamaliza.
Wamemaliza.	Hawajamaliza.

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE:

KANUSHA SENTENSI HIZI: NEGATE THE FOLLOWING SENTENCES

KWA MFANO (EXAMPLE):

Ninataka kula ugali - Sitaki kula ugali.

1) Nimeagiza _____.
2) Tumekula _____.
3) John na Maria wanataka kunywa chai _____.
4) Watoto wameagiza chakula _____.
5) Ninapenda kula samaki na viazi _____.
6) Tunapenda kutumia visu na nyuma kwa kula Chakula _____.
7) Wamerika wanapenda kula chakula kwa mikono _____.
8) Maria ameagiza sahani moja ya ugali _____.
9) John anataka glasi moja ya maji baridi _____.
10) Watoto wanapenda kunywa pombe _____.

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO.

CREATE QUESTIONS RESULTING IN THE FOLLOWING ANSWERS:

EXAMPLE:- **Mnakula ugali na nyama.**
Mnakula nini?

a) Ameagiza chai _____.
b) Unakwenda hotelini _____.
c) John na Maria wameagiza chakula _____.
d) Wanapenda kula chapati na mboga _____.
e) John anakunywa pombe baridi _____.
f) Wamekula mkate _____.

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE

SEMA KWA KIINGEREZA - SAY IN ENGLISH.

a) Ninataka kula ugali _____.
b) Nimeagiza chakula na soda baridi _____.
c) Tumemaliza kula chakula cha asubuhi _____.
d) Nipe maji ya kunywa _____.
e) Tuletee vinywaji tafadhali _____.
f) Waletee maji ya kunawa mikono _____.

ZOEZI LA NNE (EXERCISE FOUR)

USE THE "ME" TENSE IN THE FOLLOWING SENTENCES.
Example: Ninasoma - Nimesoma

a) Ninakula chakula _____.
b) Wanasoma vitabu _____.
c) Anafahamu kiswahili _____.
d) Tunajifunza kiswahili _____.
e) Watoto wanapumzika _____.

ZOEZI LA TANO - EXERCISE FIVE

KANUSHA SENTENSI HIZI - NEGATE THE FOLLOWING SENTENCES.

EXAMPLE: Nimejifunza kiswahili - Sijajifunza kiswahili.

a) Nimemaliza kula chakula _____.
b) Tumecheza mpira _____.
c) Daudi na Kamau wameshiba _____.
d) Wameagiza chakula na vinywaji baridi _____.
e) Tumepumzika baada ya kufanya kazi _____.

Cultural Note:
In most local hotels there are standards menu's written on the wall. Don't be surprised when you ask for something from the menu and you are told it is not available.

Water for washing hands is not provided in the hotels.

BEST COPY AVAILABLE

MSICHANA.

MAMA

MTOTO

BABU.

SOMO LA TISA

JAMAA YANGU - MY FAMILY

MAZUNGUMZO YA KWANZA - DIALOGUE

Njure: - Hujambo.
Ezekiel: - Sijambo sana.
Njure: - Unatoka wapi?
Ezekiel: - Ninatoka Naivasha.
Njure: - Huyu ni rafiki yako?
Ezekiel: - Hapana, huyu ni baba yangu.
Njure: - Baba yako anafanya kazi gani?
Ezekiel: - Yeye ni mkulima.
Njure: - Una dada na kaka?
Ezekiel: - Ndiyo, nina dada wawili na kaka mmoja.
Njure: - Dada zako wanafanya nini?
Ezekiel: - Wanahudhuria shule ya msingi.
Njure: - Na kaka yako anahudhuria shule pia?
Ezekiel: - Hapana yeye alimaliza shule na sasa anatafuta kazi.

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD

Baba yangu.
Baba yako.
Baba yake.
Baba yako anaitwaje?
Baba yangu anaitwa John.
Baba yako anaitwa Njuguna.
Baba yake anaitwa Musa.
Wazazi wangu wanaishi Nairobi.
Wazazi wako wanaishi Naivasha.
Wazazi wake ni Wakulima.
Wazazi wako wanaishi wapi?
Kaka yangu anafanya kazi.
Dada yake ameolewa.
Dada yao ana watoto wawili wasichana.
Wazazi wangu wamehamia Tanzania.
Nyanya na babu wangu wanakaa nyumbani.
Baba yako anafany kazi gani?
Yeye ana ndugu wengi.
Mimi sina kaka.
Wewe huna kaka.
Yeye hana babu na nyanya walifariki zamani.
Una ndugu wangapi?
Nina ndugu watatu.
Nina ndugu sita.
Baba yangu anafanya kazi.
Kaka yangu anaenda shule.
Mama yangu hafanyi kazi.
nyanya yangu alifariki.
Zamani sana.
Baba yako hufanya nini?
Baba yangu hafanyi kazi, anafanya biashara.

BEST COPY AVAILABLE

Hawa ni wazazi wa John.
Hao ni wazazi wa Maria.
Wale ni wazazi wa Susan.
Huyu ni baba yangu.
Huyo ni mama yangu.
Yule ni kaka yangu.
Hawa ni kaka na dada.

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

SWAHILI	PLURAL	ENGLISH EQUIVALENT
baba	baba	father
mama	mama	mother
mzazi	wazazi	parent
mtoto	watoto	child
kaka	kaka	brother
dada	dada	sister
mjomba	wajomba	uncle
shangazi	shangazi	aunt
babu	babu	grandfather
nyanya	nyanya	grandmother
mjukuu	wajukuu	grandchild
mke	wake	wife
mtoto wa kike	watoto wa kike	female child
mtoto wa kiume	watoto wa kiume	male child
msichana	wasichana	girl
mvulana	wavulana	boy

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION

Demonstrative Pronouns:

In this lesson demonstrative pronouns "huyu, huyo, yule" which roughly translate to English "This, that and that over there" have been used. One major difference in swahili is that where there is only one form of demonstratives in English "This" and "That" in swahili this is determined by the noun class used in a sentence. In this lesson we will deal with only demonstratives of M-WA Noun Class as follows:-

Huyu - This person (near speaker)
Huyo - That person (near the one who is addressed)
Yule - That person (at a distance from both speaker and the one addrssed.

For Example:

Huyu ni rafiki yangu. - This is my friend.
Huyo ni Peter. - That person (Near you) is Peter.
Yule ni Ezekiel. - That person (at a distance) is Ezekiel.

The Plural forms of Demonstratives are:

Hawa - These people.
Hao - Those people (near you).
Wale - Those people (distal).

Note: That linguistically demonstrative Pronouns are categorised as:

Proximal Demonstrative:
Stands in place of a person or object (see other noun classes) near the speaker.

For Example:
Proximal Demonstrative:-
Huyu ni mtoto: This (near me that I can actually touch) is a child

Refrential Demonstrative:
Stands in place of a person or object (as in above) near the person who is spoken to also, this form of demonstrative can stand in place of a person or object that is not there but has already been refered to by name.

For Example:

Ezekiel ni mwalimu. -	Ezekiel is a teacher.
Mwalimu huyo (Ezekiel)-	That teacher (referential) likes
Anapenda kufundisha.	teaching.

Distal Demonstrative:
This is used in place of an object or person that is at a distance from both the speaker and the "spoken to", but that can actual be seen an pointed at. If I can not be seen then I become a referential demonstrative as in above.

For Example:
Yule ni Bruce - That (at a distance) is Bruce

JAMAA YANGU.

Jina langu ni Njogu. Ninaishi Njoro na wazazi wangu. Baba yangu anaitwa Kamau na Mama anaitwa Wanjiku. Nina ndugu sita; kaka wanne na dada wawili. Dada yangu mkubwa ameolewa. Shangazi yangu anaitwa Wambui yeye ni mwalimu anafanya kazi mjini Nakuru. Yeye huja kututembelea kila wikendi.
Ndugu zangu wengine ni wananfunzi katika shule ya upili. Wawili watafanya mtihani wa "KCE" mwaka huu. Babu na nyanya wetu pia wanaishi na sisi kwa sababu wao ni wazee sana. Babu na nyanya hawafanyi kazi wanakaa nyumbani tu. Babu na nyanya wetu wanapenda kuzungumza na wajukuu wao kwa sababu wanawapenda sana.

JIBU MASWALI HAYA - ANSWER THE FOLLOWING QUESTIONS.

1. Njogu anaishi wapi?
2. Njogu anaishi na nani?
3. Njogu ana ndugu wangapi na wanafanya nini?
4. Shangazi wa Njogu hufanya nini?
5. Kwa nini Babu na Nyanya wa Njogu hawafanyi kazi?
6. Kaka wawili wa Njogu hufanya nini?

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO

SEMA KWA KISWAHILI -SAY IN SWAHILI.

1. I have two sisters and one brother.
2. My aunt stays in Nairobi.
3. Her parents are working.
4. My granparents died long ago.
5. His father lives in Chicago.
6. Her elder sister got married in 1976.
7. My two younger brothers go to school.
8. My father is a business man.
9. Their parent are farmers.
10. His sisters are very good.

ZOEZI LA TATU: - EXERCISE 3
JIBU MASWALI HAYA: - ANSWER THE FOLLOWING QUESTIONS:

1. Ndugu wako wa kike utamwitaje?
2. Dada ya mama yako utamwitaje?
3. Utamwitaje mtoto wa ndugu ya baba yako?
4. Ndugu wa kike wa baba utamwitaje
5. Mtoto ambaye wazazi wake wamefariki anaitwaje?
6. Baba na mama wa wazazi wako utawaitaje?
7. Baba wa kambo ni nani?
8. Wajukuu ni nani?
9. Ndugu wa kike wa baba utamwitaje?
10. Wazazi wa mke wako utawaitaje?

ZOEZI LA NNE - EXERCISE FOUR:
Unaweza kuandika Insha juu ya Jamaa yako katika Amerika - Can you write a composition about your family in Amerika.

MAELEZO YA UTAMADUNI - CULTURAL EXPLANATION.

As you may well know, Africans have extended family relations. The family includes all sorts of relatives, close and distant and as children grow up they are required to know all their relatives. And even where Africans have adopted the nuclear family model, they usually maintain close relations with other relatives. So in many cases, the minimum that will be required of you is to know something about all your existing relatives.

Naming of children varies from one ethnic group to another. If you are interesrted in knowing about any specific ethnic group talk to any of the trainers freom that particular ethnic group.

When it comes to things like pregnancy they are treated as confidential matters and people just don't talk about them freely. For more information please consult your trainers.

BEST COPY AVAILABLE

SOMO LA KUMI

NI PESA NGAPI? - HOW MUCH IS IT?

MAZUNGUMZO YA KWANZA - FIRST DIALOGUE

Ryan: Habari gani mama?
Mwuzaji: Nzuri sana. Na wewe?
Ryan: Salama tu.
Mwuzaji: Ungetaka kununua nini?
Ryan: Ningependa kununua shati. Ni pesa ngapi?
Mwuzaji: Ni shilingi mia mbili na hamsini.
Ryan: Hiyo ni bei ghali mama. Tafadhali punguza kidogo.
Mwuzaji: Hiyo ni bei rahisi, ungetaka kulipa pesa ngapi?
Ryan: Nina shilingi mia moja tu. Sina zaidi.
Mwuzaji: Basi, ongeza shiling hamsini kwa mia.
Ryan: Sawa sawa tu, chukua.
Mwuzaji: Asante. Rudi tena.

MAZUNGUMZO YA PILI - SECOND DIALOGUE

Chris: Karibu bwana. Habari yako?
Steve: Nzuri tu, unauzaje mchele?
Chris: Mchele ni shilingi ishirini kwa mkebe wa kilo moja.
Steve: Ah hiyo ni ghali sana. Punguza kidogo.
Chris: Hiyo ni bei rahisi. Ungetaka kununua kwa pesa ngapi?
Steve: Ningetaka kununua kwa shiling kumi na tano kwa mkebe.
Chris: Ikiwa nitauza kwa bei hiyo nitapata hasara. Ninahitaji faida kidogo.
Steve: Basi nitakupa shilingi kumi na sita kwa mkebe.
Chris: Hapana. Ongeza shilingi moja.
Steve: Basi chukua.
Chris: Haya. Asante rudi tena.

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD

Unauzaje nyanya.
Ninauza shilingi mbili.
Ninauza shilingi tano.
Ninauza shilingi kumi.

Viazi ni pesa ngapi?
Viazi ni shilingi sitini kwa debe.
Viazi ni shilingi mia mbili kwa gunia.
Viazi ni shiling kumi.
Karoti ni shiling hamsini kwa debe.

Unauzaje nguo?
Ninauza shiling mia mbili.
Shati ni pesa ngapi?
Ni shilingi hamsini.
Ni shilingi thelathini.

Matunda ni bei gani?
Ni shilingi mbili kwa moja.
Ni shilingi tano.
Ni shiling kumi.

Maembe ni pesa ngapi?
Ni shiling kumi.
Ni shilingi ishirini.
Ni shilingi tatu kwa moja.

Ulinunua matunda ya pesa ngapi?
Nilinunua matunda ya shiling hamsini.
Walinunua matunda ya shiling kumi.
Nilinunua matunda ya shiling tano.

Bei ya nyama ya ngombe ni ghali?
Ndiyo ni ghali sana.
Ndiyo ni ghali kidogo.
La, si ghali, ni rahisi.

Ndizi hizo ni pesa ngapi?
Ni shilingi kumi.
Ni shiling ishirini.
Ni shilingi thelathini.

Bei ya ndizi imepanda.
Bei ya vyakula imepanda.
Bei ya matunda ni ghali.

Tafadhali punguza kidogo.
Tafadhali punguza shiling moja.

Unauzaje samaki?

Ni shiling ishirini kwa kilo.
Ni shilingi kumi kwa nusu kilo.
Ni shilingi ishirini kwa kilo.

Mananasi haya ni pesa ngapi?
Ni shilingi ishirini kwa debe.
Ni shilingi kumi kwa moja.

MSAMIATI		PLURALS	VOCABULARY
rahisi		-	cheap
ghali		-	expensive
bei		-	price
mwuzaji	(M/WA)	wauzaji	seller
mnunuzi	(M/WA)	wanunuzi	buyer
bei Ghali	(Adj)	-	high price
kununua	(V)	-	to buy
bei Rahisi	(Adj)	-	cheap price

kuuza	(V)	-	to sell
faida	(Adj)	-	profit
bei ya kwaida	(Adj)	-	normal price
hasara	(Adj)	-	loss
kupata	(V)	-	to get, acquire
punguza	(V)	-	reduce/lower
kuhitaji	(V)	-	to need
ongeza	(V)	-	add
mteja	(M/WA)	wateja	customer
biashara	(N)	biashara	business
mita	(N)	mita	meter
kitambaa	(KI/VI)	vitambaa	cloth
bei Nafuu	(Adj)		better/fair price
kilo	(N)	kilo	kilogram
hadi	(Preposition)	-	until
kupiga bei	(V)	-	to bargain
bei ya Kwanza	(Adj)	-	initial/first
bei ya Mwisho	(Adj)	-	last price
kuweza	(V)	-	to be able
bidhaa	(N)	bidhaa	goods/item/things

MAELEZO YA SARUFI - (GRAMMAR EXPLANATION)

1) "NGE" TENSE:

Here the 'Nge' tense (Non-conditional) is used as a request like "Would" in this sentence.

"Would you like to buy a shirt? " Where this tense is used it is always followed by the infinitive form of a verb:

"Ungependa Kununua shati?"

NOTE: The Negative version of "ninge-"is - SINGE - Hence the Negative of a verb like :
Ningetaka would be Singetaka.

FOR EXAMPLE:

Positive: Ningetaka kwenda sokoni leo.
Negative: Singetaka kwenda sokoni leo.

All you need to do is to replace the subject makers with their corresponding negative markers.

Ningependa	-	Singependa
Ungependa	-	Hungependa
Angependa	-	Humngependa
Tunge-?	-	----------.
Mnge-?	-	----------.
Wange-?	-	----------.

For more detailed grammar explanation of or NGE, and NGALI conditional tenses, refer to your simplified Kiswahili book pages 211 - 215

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

COMPLETE THE FOLLOWING DIALOGUE:

A: Habari yako?
B: Nzuri tu. Ungetaka kununua nini?
A: _____

B: Ni shilingi mia nane na hamsini.
A: _____

B: Hiyo ni bei nzuri, lakini unaweza kulipa shilingi mia saba na ishirini.
A: _____

B: Siwezi kuchukua mia tano. Hii ni saa nzuri sana kutoka Japan.
A: _____

B: Ongeza hamsini kwa mia sita.
A: _____

B: Asante, kwaheri, rudi tena.

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO

KUUZA BIDHAA: - READING COMPREHENSION

Baba Robi anafanya kazi ya biashara. Anauza vitu tofauti kama Nguo, Matunda na vyakula. Anapata nguo kutoka Duka la Mhindi. Anauza nguo zake kwa bei ghali kwa sababu ni vigumu kupatikana, mita moja ya kitambaa ni shilingi themanini.

Yeye anauza matunda na vyakula kwa bei nafuu. Mchele kilo moja ni shiling kumi na tano. Baada ya kupiga bei, Baba Robi anaweza kupunguza bei hadi shiling kumi na mbili kwa kilo. Hii ni bei rahisi sana. Pia anauza mahindi gunia moja kwa shiling mia mbili na hamsini. Hii ni bei ya kwanza lakini baada ya kupiga bei unaweza kununua gunia moja kwa shilingi mia mbili tu. Hii ni bei yake ya mwisho lakini ni bei rahisi.

MASWALI YA UFAHAMU: READING COMPREHENSION

1. Baba Robi anafanya kazi gani?
2. Anauza vitu gani?
3. Kwa nini anauza nguo kwa bei ghali?
4. Anaweza kuuza mita tatu za kitambaa kwa pesa ngapi?
5. kwa bei rahisi, kilo moja ya mchele ni pesa ngapi?
6. Kwa bei nafuu, mchele kilo moja ni pesa ngapi?
7. Mahindi ni pesa ngapi kwa gunia moja?
8. Unapenda kazi ya Biashara? Eleza
9. Kwa nini watu wanapenda kupiga bei sokoni?

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE.

REPLACE THE PRESENT (NA) TENSE WITH THE CONDITIONAL (NGE) TENSE IN THESE SENTENCES:

Mfano - Example: Ninataka kununua matunda - Ningetaka kununua shati

1. John anapata faida kubwa baada ya kuuza mayai.
2. Unafurahi kupumzika wiki hii.
3. Tunataka kwenda Mombasa kwa Basi.
4. Wanaweza kujifunza kiswahili leo mchana.
5. Ninapenda kula chapati na kuku kesho.
6. Mnataka kutembea karibu na ziwa Naivasha?
7. Ananunua viazi kabla ya bei kupanda.
8. Tunataka kujifunza juu ya kupiga bei kesho.

ZOEZI LA NNE EXERCISE FOUR.

NEGATIVE THESE SENTENCES:

1. Ningependa kuishi katika Kenya.
2. Jeremy angetaka kuendesha baiskeli sasa.
3. Tungependa kusafiri Malindi.
4. Ningependa kununua viatu na nguo leo.
5. John na Peter wangetaka kuogelea kesho.
6. Tungetaka kujifunza juu ya Wanyama.
7. Ningetaka kutembelea Fatuma kesho.

MAELEZO YA UTAMADUNI - CULTURAL EXPLANATION:

Bargaining in African communities is part of business. It's an obligation to a stranger in a Kenyan society to learn the market vocabulary for better survival and functioning. Generally the buyer's aim is to buy at a cheaper price while the seller intends to get some profit.

Most commodities do not have prices. You need to enquire the prices before you buy or bargain. However, you cannot bargain on factory products because they have recommended prices.

SOMO LA KUMI NA MOJA

SASA NI SAA NGAPI? - WHAT IS IT NOW?

READING COMPREHENSION

Mimi ni mwalimu, hufundisha kila siku kutoka Jumatatu mpaka Ijumaa. Mimi huamka saa kumi na mbili, hujitayarisha mpaka saa moja na nusu. Hula chakula cha asubuhi saa mbili kasorobo. Masomo huanza saa mbili na nusu. Ninaishi karibu na shule kwa hivyo hutembea kwa muda wa dakika tano. Katika shule, mimi huenda kwa ofisi ya walimu, husalimiana na walimu wengine halafu sisi huenda madarasani saa mbili na nusu baada ya kengele kupigwa. Mimi hufunza somo moja kwa dakika arobaini na tano, kwa hivyo mimi hufunza masomo matatu asubuhi na mawili jioni baada ya chakula cha mchana. Mimi humaliza kufunza saa kumi na robo. Hunywa chai ya jioni halafu hupumzika na kutayarisha masomo ya siku inayofuata.

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD.

Sasa ni saa ngapi?
Sasa ni saa moja.
Sasa ni saa moja na nusu asubuhi.
Sasa ni saa nane.
Saa ngapi?
Saa tano na robo.
Saa tisa kasorobo.
Saa nne na nusu.
Saa kumi kamili.
Saa nane bado dakika kumi.

Mimi huamka saa kumi na mbili.
Wewe huanza kujifunza saa mbili na nusu.
Yeye hula chakula cha asubuhi saa moja na nusu.

Sisi hufika nyumbani jioni saa kumi na mbili na robo.
Wao huamka saa moja kasorobo.
Wao huchelewa darasani.
Wewe huamka saa ngapi?

Mimi huamka saa moja.
Wewe huamka saa kumi na mbili kasorobo.
Jumapili yeye huamka saa tatu kamili.
Sasa ni kama saa sita.
Sasa ni karibu saa tano.
Mimi huamka alfajiri.
Yeye hufanya kazi mpaka jioni.

BEST COPY AVAILABLE

MSAMIATI		VOCABULARY
saa	-	time
saa moja	-	seven o'clock
saa mbili	-	eight o'clock
saa tatu	-	nine o'clock
saa nne	-	ten o'clock
saa tano	-	eleven o'clock
saa sita	-	twelve o'clock
saa saba	-	one o'clock
saa nane	-	two o'clock
saa tisa	-	three o'clock
saa kumi	-	four o'clock
saa kumi na moja	-	five o'clock
saa kumi na mbili-		six o'clock
nusu	-	half
kasoro / bado	-	less
dakika	-	minute/minutes
saa moja na dakika tano		five minutes past seven o'clock
saa moja ya asubuhi		seven o'clock in the morning
saa moja ya usiku		seven o'clock at night
usiku		night
mchana		day time
asubuhi		morning
alfajiri		dawn / very early
alfajiri na mapema		very early in the morning
mapema		early
adhuhuri		noon / Midday
alasiri		afternoon
jioni		evening
kama		about
nukta		a second / seconds
kamili		sharp / on the dot
robo		quarter

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION

THE HABITUAL TENSE - "HU"

Unlike the other Swahili Tenses, both basic and compound tenses, the habitual tense -Hu- is not conjugated in the verb tense after a subject prefix. that is to say it does not take a subject prefix. In M-WA Noun class it is usually preceded by personal pronouns.

For Example:

Mimi Huamka	-	I usually wake up.
Wewe huamka	-	You (sing.) usually wake up.
Yeye huamka	-	S(he) usually wake up.

Positive Plural:

Sisi hufanya kazi	-	We usually work.
Nyinyi hufanya kazi	-	You (plu.) usually work.
Wao hufanya kazi	-	They usually work.

Negation:
In the negative, the habitual tense takes the characteristics of the present continous tense -Na- already explained in lesson two. However to be able to distinguish the usage of the two tenses, often the Personal Pronouns are used.

For Example:
Negative Singular:

Mimi siamki - I do not usually wake up.
Wewe huamki - You (sing.) do not wake up.
Yeye haamki - S(he) does not wake up

Negative Plural:
Sisi hatufanyi kazi - We do not usually work.
Nyinyi hamfanyi kazi- You (plu.) do not usually work.
Wao hawafanyi kazi - They do not usually work.

Note thaat in place of Personal Pronouns
Names of people as in the third person are also used with the habitual tense.

For example:
Ezekiel huamka mapema - Ezekiel usually wakes up early
and
Njure hufanya kazi Uganda- Njure usually works in Uganda.

In other noun classes, all you need to do is to say the particular noun before the verb tense.

For Example:
Basi huondoka saa moja - The Bus usually leaves at 7.00 and in negative:-
Basi haifiki mapema - The Bus does not arrive early.

Note: The habitual tense usually goes with the following phrases:-

Kila siku - Every day
Kila Jumatatu - Every monday
Kila mwezi - Every month
Kila mwaka - Every year
Kila Mara - Every time
Kwa kawaida - Usually
Mara nyingi - Many times
Mara kwa mara - Many times
Mama kwa mara - Often
Mara nyingine/wakati mwingine - Sometimes

Minutes past the hour are usually counted up to 30, for example,

7.15 - saa moja na robo (quarter) or
saa moja na dakika kumi na tano.

7.20 - Saa moja na dakika ishirini.

7.30 Saa moja na nusu (half) or saa moja na dakika thelathini. From 31 mins onwards, minutes to the following hour are given with the word "kasoro" or bado, for example.

8.40 - Saa tatu kasoro/bado, for example dakika ishirini, 8.45 saa tatu bado robo.

8.55 - saa tatu kasoro/bado dakika tano.

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

SEMA KWA KISWAHILI - SAY IN SWAHILI
KWA MFANO - For Example

8.30 a.m. - Saa mbili na nusu asubuhi

a) 10.10 a.m._____
b) 12.00 noon_____
c) 6.30 p.m._____
d) 12.10 p.m._____
e) 5.00 p.m._____
f) 3.15 p.m _____
g) 5.45 p.m._____
h) 9.00 p.m._____
i) 10.30 p.m._____
J) 12.00 p.m._____
k) 1.30 p.m._____
l) 6.25 a.m._____
m) From 2.00 p.m. to 5.00 p.m._____

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO

JIBU MASWALI HAYA - ANSWER THE FOLLOWING QUESTIONS

1. Masomo huanza saa ngapi katika shule?
2. Mwalimu huenda vipi shuleni?
3. Mwalimi hufunza somo moja kwa dakika ngapi?
4. Mwalimuu hufunza masomo mangapi asubuhi na jioni?
5. Mwalimu humaliza kufundisha saa ngapi?

ZOEZI - EXERCISE THREE

Jibu maswali haya Answer the following questions

a) Wewe huenda darasani saa ngapi?
b) Masomo ya kiswahili huanza saa ngapi?
c) Wewe humaliza kujifunza saa ngapi?
d) Wewe hufika nyumbani saa ngapi?
e) Wewe hula chakula cha asubuhi saa ngapi?
f) Katika Amerika watu hula chakula cha jioni saa ngapi?
g) Katika Amerika watu hufanya kazi kutoka saa ngapi mpaka saa ngapi?

CULTURAL NOTES:

Originally Africans had no watches and thus used the sun or the shadow. Even now, elderly people may look at these and will tell time. In most cases the difference from a watch might be plus/minus fifteen minutes or so.

Note:
TIME IN SWAHILI: is based on twelve hours of daylight and twelve hours of darkness. Since the sun usually rises at 6.00 a.m., 7 a.m. is the first hour of daylight. Similarly, the sun generally sets between 6.00 p.m. and 7.00 p.m.
Swahili time and English time are just six hours different. So to arrive at one, six hours are either added or subtracted from the other. So when giving time in Swahili, the word "saa", meaning "o'clock', always precedes the time. for example. Saa moja, saa mbili, saa tatu etc.

If you ask some one to meet you at 2.00 and the person comes at 2.59 that is fine because it is still within the hour.

SOMO LA KUMI NA MBILI

LEO NI SIKU GANI? - WHAT DAY IS IT?

READING COMPREHENSION

A. John na Mary ni watoto wa Mzee Kamau. Sasa ni wakati wa likizo na wanakaa nyumbani. Kila Jumatatu wao hupenda kusaidia baba yao shambani. Jumanne Mary hufua nguo halafu siku za Jumatano Juma hupiga pasi. Alhamisi watoto huenda katika maktaba ya mji kusoma vitabu na magazeti. Watoto hawa wanapenda siku za Ijumaa kwasababu wao huenda kutembelea nyanya yao. Wao hukaa kwa nyanya mpaka Jumamosi jioni halafu wao hurudi nyumbani. Jamaa ya mzee Kamau ni wakristo, kwa hivyo wao huenda kanisani Jumapili kuomba. Kesho itakuwa Jumamosi. John na Mary watarudi kwa nyanya kusema kwaheri kwasababu wiki ijayo wataenda shule kuanza muhula wa kwanza. Kwa kawaida muhula wa kwanza huanza Januari mpaka Aprili, muhula wa pili Mei mpaka Agosti na muhula wa mwisho ni Agosti mpaka Novemba. Watu wengi hupenda mwezi wa Desemba kwasababu kuna sikukuu ya Krismasi.

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD.

Leo ni siku gani?.
Leo ni Jumamosi. Leo si Jumamosi.
Leo ni Ijumaa. Leo si Ijumaa.

Jana ilikuwa siku gani?.

Jana ilikuwa Jumapili. Jana haikuwa Jumapili.
Jana ilikuwa Jumanne. Jana haikuwa Jumanne.

Kesho itakuwa siku gani?.
Kesho itakuwa Jumatano. Kesho haitakuwa Jumatano.
Kesho itakuwa Alhamisi. Kesho haitakuwa Alhamisi.

Juzi ilikuwa Jumamosi. Juzi haikuwa Jumamosi.
Juzi ilikuwa Jumatatu. Juzi haikuwa Jumatatu.
Juzi ilikuwa Alhamisi. Juzi haikuwa Alhamisi.

Mwezi huu.
Mwezi ujao.
Mwezi uliopita.
Mwezi wa kwanza. - Januari.
Mwezi wa pili. - Februari.
Mwezi wa tatu. - Machi.
Mwezi wa nne. - Aprili.

MSAMIATI PLURAL VOCABULARY

jumatatu	(N)	-	Monday
jumanne	(N)	-	Tuesday
jumatano	(N)	-	Wednesday
alhamisi	(N)	-	Thursday
ijumaa	(N)	-	Friday
jumamosi	(N)	-	Saturday
jumapili	(N)	-	Sunday
kanisa	(MA)	makanisa	church
msikiti	(MI)	misikiti	mosque
mkristo	(M/WA)	wakristo	Christian
muisilamu	(M/WA)	waisilamu	Muslim
januari	(N)	-	January
februari	(N)	-	February
machi	(N)	-	March
aprili	(N)	-	April
mei	(N)	-	May
juni	(N)	-	June
julai	(N)	-	July
agosti	(N)	-	August
septemba	(N)	-	September
oktoba	(N)	-	October
novemba	(N)	-	November
sikukuu	(N)	-	holiday
krismasi	(N)	-	Christmas
mwezi	(MI)	-	month
mwaka	(MI)	-	year
wiki	(N)	-	week
siku	(N)	-	day
juzi	(N)	-	day before yesterday
kesho	(N)	-	tommorrow
kesho-Kutwa	(N)	-	day after tommorrow

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION

1) THE VERB "TO BE": in verb form appears in two ways in Kiswahili, namely as:

a) Ni, which is used only in the present and

b) "kuwa" which is used in all other tenses.

Ni has already been covered in earlier lessons.

2) KUWA

This is a monosyllabic verb and as such it is subject to all the rules pertaining to monosyllabic verbs both in affirmative and negative constructions. Hence from the present tense: We get

Leo ni Jumamosi - Today is Saturday.

PAST: Jana ilikuwa Jumamosi. (Yesterday was Saturday)

FUTURE: Kesho itakuwa Jumamosi. (To-morrow will be Saturday)

From the negative we get:
PAST : Jana haikuwa Jumamosi.
(Yesterday was not Saturday.)

FUTURE: Kesho haitakuwa Jumamosi.
(Tomorrow will not be Saturday.)

"Kuwa" is also used in other forms as we shall see in other lessons.

3) GENERAL RELATIVES: Usually have no tense sign as such and instead the relative like in (mwezi ujao) is added to the end of the verb stem as a suffix. The normal subject prefix is added directly on to the verb stem. This construction is very commmonly used to translate the word "next" (for example, the one which comes).

General relatives are:

For M/MI Class	(this year)	mwaka Huu
	(next year)	" Ujao
	(last year)	" uliopita
For N Class	this week	wiki Hii
	last week	iliyopita
	next week	ijayo

For example:

Mwezi ujao	-	Next month (the month which will come(s)
Mwaka ujao	-	Next year (the year which will come(s)
Wiki ijayo	-	Next week (the week which come(s)
Alhamisi ijayo	-	Next Thursday (Thursday which will come(s)

4) M/MI CLASS DEMONSTRATIVES - We have already covered demonstratives in N and M/Wa class. We will now look at demonstratives in M/MI class. These are as follows:

M/MI CLASS DEMONSTRATIVES

Singular		Plural
Huu	-	Hii (near speaker)
Huo	-	Hiyo (near listener)
Ule	-	Ile (far from both speaker and listener)

for example.	Mti huu	-	This tree
	Mti huo	-	That tree
	Mti ule	-	That tree over there
Plurals -	Miti hii	-	These trees
	Miti hiyo	-	Those trees
	Miti ile	-	those trees over there

N - CLASS

Singlar	Plural
Hii	Hizi
Hiyo	Hizo
Ile	Zile

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISES ONE.

JIBU MASWALI HAYA - ANSWER THE FOLLOWING QUESTIONS:

1. Wewe huenda kazini siku gani?
2. Wakenya wanakwenda kazini siku gani?
3. Wanafunzi hupumzika kazini siku gani?
4. Ulifika hapa Kenya siku gani?
5. Wewe hufanya nini Jumapili?
6. Leo ni siku gani?
7. Kesho itakuwa siku gani?
8. Jana ilikuwa siku gani?
9. Juzi ilikuwa siku gani?

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO

JIBU MASWALI HAYA KATIKA SENTENSI
MAKE COMPLETE SENTENCES IN ANSWER TO THE FOLLOWING QUESTIONS:

Mfano - Example

QUESTION: Mwezi wa mwisho ni mwezi gani?
ANSWER : Mwezi wa mwisho ni mwezi wa Desemba

1. Mwezi wa kwanza ni mwezi gani?
2. Februari ni mwezi wa ngapi?
3. Novemba ni mwezi wa ngapi?
4. Marchi ni mwezi wa ngapi?
6. Mwezi wa kumi ni mwezi gani?
7. Mwaka mmoja ni miezi mingapi?

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE

CONSTRUCT SENTENCES USING WORDS FROM EACH COLUMN
EXAMPLE

Jumatano	John	**husoma**
Jumatatu	-	huenda kanisa
Jamatano		husoma
Jumapili	John	hulima shambani
Alhamisi		huogelea baharini
Jumamosi		hutembelea rafiki
Jumanne		hucheza gita
Ijumaa		hupumzika

ZOEZI LA NNE - EXERCISE FOUR

JIBU MASWALI HAYA: - ANSWER THESE QUESTIONS

BEST COPY AVAILABLE

1. Leo ni siku gani?
2. Kesho itakuwa siku gani?
3. Jana ilikuwa siku gani?
4. Kesho kutwa itakuwa siku gani?
5. Juzi ilikuwa siku gani?
6. Huu ni mwezi gani?
7. Mwezi ujao utakuwa mwezi gani?
8. Mwezi uliopita ulikuwa mwezi gani?
9. Huu ni mwezi gani?
10. Huu ni mwaka gani?

MAELEZO YA UTAMADUNI - CULTURAL NOTES:

The days of the week are taken from the arabic calendar in which Friday (Ijumaa) is the most important day. Therefore the first day of the week is Saturday (Jumamosi). Mosi meaning one. However, for most ethnic groups in Kenya the first day of the week is Monday.

BEST COPY AVAILABLE

SOMO LA KUMI NA TATU

UNA UMRI GANI? - HOW OLD ARE YOU?

MAISHA YA TIM: READING COMPREHENSION

Tim alizaliwa tarehe thelathini mwezi wa mei mwaka wa elfu moja mia tisa na sitini na tatu. Sasa ana umri wa miaka ishirini na saba. Alizaliwa katika mji wa Naivasha nchini Kenya. Alikaa mjini Naivasha mpaka alipokuwa na miaka minne. katika Naivasha baba yake alifanya kazi ya kufundisha. katika mwaka wa sitini na saba, wazazi wa Tim walihama Naivasha wakaenda Nairobi.

Huko Nairobi, Tim alianza Shule ya Msingi. Baada ya miaka minane, alimaliza shule ya msingi, akaingia shule ya sekondari, katika mwaka wa elfu moja mia tisa na themanini alihudhuria chuo kikuu cha Nairobi. Huko alijifunza juu ya sayansi ya siasa.

Alipohitimu alifanya kazi kidogo katika Nairobi halafu akaenda nchi ya Ufaransa kwa masomo zaidi. Huko Ufaransa Tim alijifunza kifaranza kidogo. Baadaye alirudi kenya, akaendelea na masomo kidogo halafu alapata shahada yake mwaka wa themanini na nne. Tim alifurahi sana kwa sababu alianza kuishi peke yake,kujitengemea na kuwa na maisha mapya.

Tim alianza kutafuta kazi lakini hakupata mara moja. Baada ya miezi minne, alianza kazi ya kufundisha katika shule ya upili. Baadaye alijiriwa na serikali kama afisa wa Elimu. Sasa yeye ana cheo kikubwa, anapata mshahara mkubwa na anatarajia kujiunga na siasa mwaka ujao.

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD.

Una miaka mingapi?	Nina miaka thelathini. Nina miaka ishirini. Nina miaka ishirini na mitano.
Una umri gani?	Nina umri wa miaka arobaini. Nina umri wa miaka sabini. Nina umri wa miaka ishirini.
Juma ana miaka mingapi?	Ana miaka kumi na miwili. Ana umri wa miaka kumi na miwili.
Baba yangu ana miaka arobaini.	Ana umri wa miaka arobaini. Mama yangu ana miaka thelathini. Baba yangu ana miaka sabini.
Ulizaliwa lini?	Nilizaliwa mwaka wa 1948. Nilizaliwa mwaka wa 1968. Nilizaliwa mwaka wa 1971.

BEST COPY AVAILABLE

Ulizaliwa mwaka gani?

Nilizaliwa mwaka wa 1960.
Nilizaliwa mwaka wa 1963.
Nilizaliwa mwaka wa 1965.

Mama yako alizaliwa lini?

Alizaliwa mwaka wa 1946.
Alizaliwa mwaka wa 1936.
Alizaliwa mwaka wa 1949.

Kaka yako alizaliwa tarehe ngapi?

Alizaliwa tarehe 12 June, mwaka wa 50.

Siku yako ya kuzaliwa ni lini?.

Siku yangu ya kuzaliwa ni tarehe 18 mwezi wa Januari.

Siku yangu ya kuzaliwa ni tarehe 20 Julai.

Utaishi Kenya kwa muda gani?

Nitaishi kenya kwa muda wa mwaka mmoja.
Nitaishi kenya kwa muda wa miaka miwili.
Nitaishi Kenya kwa muda wa miezi tisa.

Utajifunza Kiswahili kwa muda gani?

Nitajifunza kiswahili kwa miezi mitatu.
Nitajifunza kiswahili kwa miezi sita.
Nitajifunza kiswahili kwa miaka miwili.
Nitajifunza kiswahili kwa muda mrefu.

Nitahudhuria shule ya msingi mwaka ujao.
Nilihudhuria shule ya sekondari mwaka wa 1980.
Nimehudhuria chuo kikuu kwa muda wa miaka miwili.

MSAMIATI		MISAMIATI	VOCABULARY
maisha	(n)	maisha	life
kuzaliwa	(v)	kuzaliwa	to be born
umri	(n)	umri	age
tarehe	(n)	tarehe	date
mwaka	(n)	miaka	year
mwezi	(n)	miezi	month
kuhama	(v)	-	to migrate
elimu	(n)	elimu	education
kuanza	(v)	-	to start
kuhamia	(v)	-	to migrate to
kumaliza	(v)	-	to finish
shule ya msingi	(n)	shule ya msingi	primary school
shule ya upili	(n)	shule za sekendary	secondary school
kuhudhuria	(v)	-	to attend
kuhitimu	(v)	-	to graduate
chuo kikuu	(v)	vyou vikuu	university
kifaransa	(n)	-	French
kuendelea	(v)	-	to continue
pekee		-	above

siku ya kuzaliwa		-	birthday
mtihani	(n)	mtihani	exam
kufaulu	(v)	-	to succeed
kupita	(v)	-	to pass
shahada	(n)	shahada	degree/certificate
ingia	(v)	-	enter
kutafuta	(v)	-	to look for
kuajiriwa		-	to be employed
kujiunga		-	to join
kujitegemea		-	to depend on one self
lini"		-	when

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION

The Narrative tense -Ka-.
The narrative -ka- is used in swahili to show a series of events happening one after the other. It can be compared to English "and then" or "then" when narrating a story as in "I woke up, dressed then left for work". Before using the -ka- narrative in a sentence, the first verb is in the past tense -Li-.

For Example:
Niliamka nikavaa halafu nikaenda kazini.- I woke, dressed and then went to work.

As a tense marker the narrative tense has the same characteristics as other swahili tenses i.e. it comes after the subject prefix.

For Example:
Nikaamka. - (and then) I woke up.
Ukaamka. - (and then) you woke up.
Akaamka - (and then) S(he) woke up etc.
However, the narrative tense does not have a negative tense marker but uses the past tense negative -Ku- explained in earlier lessons.

The Adverb of time -Po-
The Adverb of time -Po- is used in Swahili like in English 'when' as in "when I was in School". In a verb tense it is inserted between a tense marker and the action verb.

For Example: In Present Tense Action Verb
Ninaposoma. - When I read.
Unaposoma. - When you read.
Anaposoma. - When s(he) reads.

Note that: The Adverb of time -Po- is only used in three time frames; i.e. the present tense -Na-, the past tense -Li- and the future tense -Ta-.

For Example:
In the past tense we get:-
Nilipoamka. - When I woke up.
Ulipoamka. - When you woke up.
Alipoamka. - When he/she woke up.

BEST COPY AVAILABLE

However, in the future tense - Ta- an extra element -Ka- is inserted to form -Taka-.

For Example:

Nitakapoenda.	-	When I will go.
Utakapoenda.	-	When you will go.
Atakapoenda	-	When s/he will go.

NOTE: In the examples, the word "and" is not translated. This is because the sense of 'and' is already conveyed by the tense sign "-ka-".

(another exampale here)

- This tense must however be introduced by an ordinary past tense.

The -Ki- tense marker denotes an action that was or will be in a continous state in Swahili as in English "I was working" "I will be working and "I have been working". Usually in the construction of this sentence, the first verb is the verb to be "KUWA".

For Example:

Nilikuwa nikisoma.	-	I was reading.
Ulkuwa ukisoma.	-	You were reading.
Alikuwa akisoma.	-	S/he was reading.

In some cases the present continous tense -Na- is used in place of -Ki- to give the same meaning:

For Example:

Nilikuwa ninasoma.	-	I was reading.
Ulikuwa unasoma.	-	You were reading.
Alikuwa anasoma.	-	S/he was reading.

In the negative, there are two ways of negating the continous state in a verb tense. You can negate the first or the second verb.

For Example:

Nilikuwa sisomi.	-	I was not reading.
Ulikuwa husomi.	-	You were not reading.
Alikuwa hasomi.	-	S/he was not reading

or

Sikuwa nikisoma	)	
Hukuwa ukisoma	)	See above English meaning.
Hakuwa akisoma	)	

For more explantion of the -po- tense refer to Simplified Swahili pages 184-185.

For more details on the 'ka' tense refer to Simplified Swahili pp 207-211.

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

(Read the passage at the beginning of the lesson and answer the following questions).
Jibu maswali haya - Answer these questions.

1. Tim alizaliwa lini? _____
2. Alizaliwa wapi? _____
3. Alikwenda shule ya msingi lini _____
4. Wazazi wake walihamia wapi? _____
5. Baba yake alifanya kazi gani? _____
6. Alihudhuria chuo kikuu lini? _____
7. Alijifunza nini katika chuo kikuu? _____
8. Baada ya kuhitimu Tim alifanya nini? _____
9. Kwa nini Tim alienda Ufaransa? _____
10. Alipata shahada mwaka gani? _____
11. Kwa nini alifurahia kupata shahada? _____
12. Baada ya miezi minne alipata kazi gani? _____
13. Aliajiriwa na serikali kufanya kazi gani? _____
14. Mwaka ujao Tim atafanya nini? _____
15. Tim ana miaka mingapi sasa? _____

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO

JIBU MASWALI HAYA - ANSWER THE FOLLOWING QUESTIONS:.

a) Wewe una umri gani? _____
b) Ulizaliwa mwaka gani? _____
c) Ulizaliwa mji gani? _____
d) Wazazi wako wanaishi wapi? _____
e) Ulianza shule lini? _____
f) Ulienda shule ya sekondari kwa mda gani? _____
g) Ulihudhuria chuo kikuu lini? _____
f) Ulijifunza chuo kikuu kwa mda gani? _____
h) Ulianza kujifunza kiswahili lini? Kwa nini unajifunza kiswahili? _____
i) Umejifunza kiswahili kwa mda gani? _____
k) Utakaa kenya kwa mda gani? _____
l) Andika juu ya maisha yako _____

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE.

Use: Ka' Narrative Tense in the following sentenses:

1. Mwanafunzi alikwenda ofisini alipata barua.
2. Nilifiamka asubuhi, nilioga na nilikunywa chai.
3. Tulijifunza jana usiku tulichoka sana halafu tulilala mapema.
